



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



Kumb. Na. AB.113/388/95

Tarehe: 14 Machi, 2023

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb.Na. FA.170/374/01 "A"/140 cha tarehe 16 Februari, 2023 kilichotolewa na Katibu Mkuu (UTUMISHI) anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi Nne (04) kama ilivyoanishwa katika Tangazo hili, kwa sifa zifuatazo:-

#### 1.0 MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA LA II - NAFASI 1

##### 1.1 SIFA:

- Awe amehitimu na kupata Cheti cha Kidato cha Nne wenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili. Aidha, awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 80 kwa dakika moja na kupata program za kompyuta za ofisi kama vile: Word, Excel, Powerpoint, internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### 1.2 KAZI NA MAJUKUMU

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri.
- Kupokea wageni na kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miradi, wageni na tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba za kazi nyingine.
- Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika.
- Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali; na
- Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi.

##### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA

- Mwombaji atakayefanikiwa kuajiriwa kwa cheo cha Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la II atalipwa mshahara ngazi ya TGS C/1 kwa mwezi.

## 1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI 3

### 2.1 SIFA:

- Awe amehitimu na kupata Cheli cha Kidato cha Nne mwenye Stashahada (NTA level 6) katika fani ya urasimu ramani (cartography) au (geoinformatics), sharia, afya au masijala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali mwenye ujuzi wa kompyuta.

### 2.2 KAZI NA MAJUKUMU

- Kuorodhesha barua zinazolingia masijala kwenye regista
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi
- Kusambaza majalada kwa Watendaji
- Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa Watendaji
- Kutafuta kumbukumbu, nyaraka/ majarada yanayohitajika na Watendaji
- Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada yanapohifadhiwa
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi

### 2.3 NGAZI YA MSHAHARA

- Mwombaji atakayefanikiwa kuajiriwa kwa cheo cha Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II atalipwa mshahara ngazi ya TGS C/1 kwa mwezi.

### MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18-45
- Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- Barua ya muombaji ioneshe anuani anayotumia kwasasa pamoja na namba ya simu ikiambatana na:
- Nakala za vyeti vya taaluma
- Nakala ya vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa na kazi husika.
- Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- Picha mbili (2) za "Passport Size" za hivi karibuni.
- Kitambulisho cha Taifa au namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- Waombaji waliowahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiliwa
- "Testmonies", "Provisional Result", "Statement of results" hati ya matokeo ya Kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULT SLIPS HAVITAKUBALIWA.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE)

- xii. Waombaji waliostaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi
- xiii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahasika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xiv. Waombaji wenye sifa zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa.

Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha maombi yao katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo au kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi wa Manispaa,  
Manispaa ya Ubungo,  
S.L.P 55068.  
DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29/03/2023 Saa 9:30 Alasiri**

**NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri  
[www.ubungomc.go.tz](http://www.ubungomc.go.tz)**

  
Beatrice R. Dominic  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
MUNICIPAL DIRECTOR  
UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL  
DAR-ES-SALAAM